

ENTREPRENEURS...



Vibindo na ugumu wa kurasimisha biashara

Mwandishi Wetu, Mwananchi

Kila mara wenye biashara ndogo hukabiliwa na maswali kuhusu usajili wa shughuli zao. Wafanyabiashara hawa ukiwahoji wanasema wazi kwamba hujiuliza maswali kama wasajili/warasimisha biashara zao au waache.

Watu hawa hujiuliza wanafaidika nini kwa kusajili au kutosajili biashara.

Mwenyekiti wa Vibindo nchini, taasisi inayowasilisha wafanyabiashara wadogo zaidi ya 50,000, Gaston Kikuwi, anasema wanachama hawaoni faida wala sababu ya kusajili biashara zao.

“Tafiti zilizopo zinaonyesha kwamba wafanyabiashara wengi wadogo wanataka kusajili biashara zao, lakini gharama zipo juu, huku wakusanya kodi wakitaka kodi kubwa kabla ya kuanza kwa shughuli husika,” anasema.

Faida ya kusajili

Kwa sasa mtu anaona faida ya kusajili shughuli yake iwapo anataka fedha au huduma za kifedha na soko rasmi la shughuli yake kama zabuni. Lakini wafanyabiashara wadogo wasiohitaji huduma za fedha kama mikopo, hawaoni haja ya kusajili shughuli zao.

Kikuwi anasema Vibindo inataka Serikali mpya kuangalia changamoto za wenye biashara wadogo katika hilo na kuachana na sheria ya usajili wa biashara.

SAUTI ZA WANANCHI

Mwalimu Patric Maro wa Shule ya Sekondari Kashai, Bukoba

Anasema kuwa tukitaka kuendeleza sekta ya viwanda tunatakiwa tujikite zaidi na shule za ufundi na elimu ya kujitegemea.

Kwa namna hii tutakuwa na watu wengi ambao wanajikita katika maeneo wanayoyajua kwa undani zaidi katika fani mbalimbali za viwandani, na hivyo kutengeneza nafasi za kazi.

Aidha, Serikali ichukue hatua madhubuti za kuokoa anguko la shilingi. Katika migodi, iruhusu benki za ndani kununua madini kutoka kwa wachimbaji wadogo na kuyauza badala ya wachimba madini wenyewe kutafuta soko kwa kuwa wanaweza kudanganywa na wachuuzi wakubwa.

“Hali hiyo itasaidia pia benki za ndani kuwa na akiba kubwa ya fedha za kigeni ambayo pia wataitumia kuwawezesha wawekezaji kama mtaji, kwa hiyo kuongeza tija. Kwa kitendo hiki kutakuwepo na ongezeko la fedha za kigeni na hivyo kuongeza nguvu ya shilingi, anasema Egbeth Leon wa Dar es Salaam.

“Sheria hii si rafiki kwa wafanyabiashara wadogo. Haileti mvuto wa mtu kwenda kusajili biashara yake. Wafanyabiashara wadogo wanataka sheria ambayo itawavuta kwenye usajili. Wafanyabiashara wanataka serikali kuiondoa sheria ya sasa, lakini juhudi zifanyike kuimarisha wakala wa usajili wa biashara na leseni (Brela) ili kufikia mikoa yote nje na Dar es Salaam,” anaeleza na kuongeza:

“Tunaitaka Serikali mpya kuanzisha majadiliano kuhusu usajili wa biashara. Ni muhimu kama Serikali mpya itahitaji mamilioni ya watu kusajili biashara kufuta sheria hiyo ya usajili na kurejea tena utoaji leseni za biashara.”

Kwa mujibu wa Vibindo, tangu mwaka 2007 wamekuwa wakionyesha changamoto mbalimbali zinazofanya sheria hiyo isitekelezwe.

Miaka 10 ya uraghibishi

Kwa miaka 10 Vibindo imekuwa ikiambia Serikali kama inataka kuboresha mazingira ya biashara na kupunguza gharama za kufanya biashara, kuna haja ya kubadilisha sheria hiyo ya usajili wa biashara.

“Sheria hii ina athari mbaya kwa biashara nchini,” anasisitiza Kikuwi na kuongeza kuwa itakuwa ni vyema kama Serikali mpya itayachukulia maanani masuala ambayo wamekuwa wakiyapendekeza kwa miaka 10 sasa.

Ofisa mtendaji wa zamani wa Brela, Estario Mahingila anasema kwamba asilimia 20 tu ya watu ndio wanaolipa kodi. Hali hiyo inatokana na watu wengi kutosajili biashara zao au kutokuwa na leseni.

Ofisa Mtendaji mkuu wa Taasisi ya utafiti wa kupunguza umaskini (REPOA) Profesa Samuel Wangwe, anaamini kwamba wafanyabiashara hawana sababu za kusajili biashara zao kwa kuwa hakuna kitu muhimu wanachoweza kukipata kwa kusajili biashara zao.

“Tatizo ni kuwa Serikali inawaambia wananchi kwamba wanataka wajisajili ili waweze kuwalipisha kodi, badala ya kuwaambia kwamba wafanye hivyo ili waweze kupata huduma za kuendeleza biashara zao,” anasema.

Anasema kama wenye biashara hao wataelezwa wakaelewa

umuhimu wa kusajili, watajisajili na Serikali itaongeza pato lake.

“Ni vyema Serikali ikawa na mizania kuhusu gharama na faida ya kufanya biashara iliyosajiliwa. Ni vyema ikatumia vitu vinaavyoweza kuwavuta watu kujisajili kwa kutoa taarifa mbalimbali na huduma za jamii,” anasema Profesa Wangwe.

Naye Mhadhiri mwandamizi wa uchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Humphrey Moshi, anasema kwamba kama asilimia 50 ya biashara ambazo hazijasajiliwa zikisajiliwa pato la taifa linaweza kuongezeka kwa asilimia 10.

Anasema biashara ndogo na za kati zinaendelea kutambulika kama ndizo zinazokuza uchumi katika nchi nyingi, zinatambulika kama ndio funguo ya kuendesha uchumi na ajira.

“Serikali ya Tanzania ni lazima ifanye kazi usiku na mchana kushawishi wafanyabiashara wasajili biashara zao,” anasema na kuongeza:

“Serikali inatakiwa kuangalia usajili wa biashara ndogo kama chombo cha kuwatambua, hali ambayo itawezesha biashara nyingi zaidi kujisajili na kuongeza pato la Taifa.”

Wasiwasi wa VIBINDO

Sheria ya usajili wa biashara, ina weka wazi kuhusu mamlaka kumpatia leseni mfanyabiashara lakini upatikanaji wake unafanyika tofauti na inakatisha tamaa. Upatikanaji wa leseni huchukua muda na kuna urasimu mkubwa.

Sheria imejijenga katika usajili wa mambo yanayofanyika katika biashara husika badala ya majina au uanzishaji wa taasisi au uanzishaji wa biashara. Na hii inaweza kuleta usajili mara mbili wa biashara.

Utekelezaji wa sheria hiyo ni changamoto kubwa, mathalani sheria hiyo kifungu cha 7 (1) kunataka kuanzishwa kwa vituo vya kusajili biashara katika kila mamlaka za utawala wa mikoa na serikali za mitaa. Katika ngazi ya kijiji, hilo ni kama haliwezekani, sheria inastahili kufanyiwa mabadiliko angalau usajili uwe wa ngazi ya wilaya.

Sheria hii inasimamiwa na wizara mbili, Tamisemi na wizara ya biashara viwanda na masoko. Kutokana na kwamba kila wizara ina malengo na sera zake, wakati mwingine kunatokea mgongano na ukosefu wa uwajibikaji.

Sheria hiyo inatengeneza michakato mingi ya upatikanaji wa leseni na kuongeza gharama za kuendesha biashara.

Andika na tuma maoni yako katika ujumbe mfupi (SMS) kwenye simu namba 0786240172.

Tuambie unafikiria nini ili kuboresha mazingira ya biashara nchini. Mrejesho wako unathaminiwa sana. Tunatoa muda wa maongezi wa shilingi elfu 30 kwa kila ujumbe tutakouchapisha.

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA

BEST-Dialogue



Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo